


# “BIBLIA KATIKA DAKIKA TANO (5)"

Hujambo! Nakusalimu asubuhi ya leo.

Katika Machapisho yetu ya awali, tulijadili Yesu-Aliye, ama Yesu halisi. Huu ungali ndio mwanzo wa kuuchunguza utajiri wa Yesu Halisi! Mungu akipenda, hivi karibuni tutarejea kwenye mada hii.

Lakini sasa ningependa kuchukua mda ili kukueleza kwa nini tunafanya hivi.

Ninapofundisha barani Afrika napenda kuanza na “Biblia ya Dakika 5”.

Watu wengi wanaokuja kunisikia nikizungumza hawanijui. Wanakuja kwa sababu mbalimbali; wengine ili kudadisi, wengine kwa mwaliko wa watu wanaowajua, qengine kwa sababu hawana chochote kingine cha kufanya siku hiyo, na pia labda kwa chakula cha mchana cha bure!

Lakini tunaamini wengi wanakuja kwa sababu wanavutwa na Roho Mtakatifu.

Lakini kwa nini wanisikilize? Kwa nini wamsikilize huyu mzungu kutoka Marekani?
Angeweza kusema nini ambacho ni muhimu kwa wanaume na wanawake wa Kiafrika wanaojitahidi kuwatoa wengine gizani na kuwaleta katika nuru - huku wakihangaika kuzilisha familia zao?

Haya ni maswali mazuri. Lakini kwanza nauliza swali hili.

“Ikiwa ninaweza kufanikiwa kufundisha Biblia nzima kwa dakika tano, je, mtasikiliza mambo mengine nitakayokuja kushiriki?” Changamoto hiyo huamsha tabasamu nyingi lakini wasikilizaji wenye neema hunipa ruhusa kila wakati kujaribu. Angalia saa kwenye saa yako. Hebu tuone kama ninaweza kuifanya. Twende sasa….

“Biblia ina aina nyingi za fasihi: historia, mashairi, nyimbo, unabii, maadili
mafundisho, hekima, mafumbo, ufunuo, na mengineyo. Kuisoma Biblia ni changamoto kwa wengi. Baadhi ya sehemu hata hazijapangwa kwa mpangilio wa matukio!"

"Kwa hivyo ni nini kinachogeuza maandishi haya 66 tofauti kuwa 'Byblos'(Kigiriki) - Kitabu Kimoja - Biblia Moja Takatifu? Ni mada gani inayounganisha hadithi kuu ya Biblia kutoka Mwanzo hadi Ufunuo ambayo Mungu anajribu kutuambia?

“Ndiyo hii hapa. Angalia ikiwa unakubali...

“Kutoka katika moyo wa upendo na kwa nia ya upendo, Mungu aliuumba ulimwengu mzima. Kisha aliining'iniza sayari yetu ndogo angani mahali fulani karibu na kitovu cha bahari hii kuu nyota na sayari na galaksi."

"Na kisha akaijaza sayari ndogo ya Dunia na kila aina ya uhai - na vile vile
aina nyingine za maisha zisizofikirika.

"Na kisha kama kilele cha uumbaji wake, alituumba sisi - watu - akatupa ubinadamu. Sisi ndio kilele cha uumbaji wake kwa sababu, kwa kadri tujuavyo, ni sisi pekee katika ulimwengu ndio tulioumbwa kwa mfano wa Mungu mwenyewe.

“Kuumbwa kwa mfano wa Mungu kunamaanisha mambo mengi. Tumeundwa kama daraja kati  ya ulimwengu wa asili unaoonekana na ulimwengu wa kiroho usioonekana. Tumeumbwa kuishi katika hali zote mbili kwa wakati mmoja. Tumeumbwa kuusimamia ulimwengu wa asili. Tumeumbwa kuishi milele ndani ya ulimwengu wa kiroho.

"Kwa hivyo - jiulize hili - kwa nini Mungu aliwekeza wakati mwingi, nguvu, katika jambo hili?

"Biblia inatuambia jibu - tafakari kama unaweza kutambua nyuzi zinazoshikanisha kitabu cha Mwanzo na kitabu cha Ufunuo.

“Kutoka katika moyo wa upendo, kwa nia ya upendo, Mungu anajitengenezea Watu wa kipekee - Watu wanaoitwa kwa Jina lake - Watu wanaotambua na kuakisi utukufu wake - Watu ambao Anakuja kukaa ndani yao - sasa na hata milele.

"Hiyo ndiyo Hadithi Kubwa. Haya ndiyo Mungu anayafanya duniani. Hivyo ndivyo Biblia inavyojifunua kwetu. Mungu anazisongeza mbingu na nchi ili kujitengenezea Watu - Watu wanaomjua Yeye - kumpenda - kumwabudu - kumtii - kumtumikia - kumwakilisha - na kumfurahia - sasa na hata milele.

“Ndiyo hivyo. Mungu aliumba vitu vingine vyote ili aweze kutuumba. Kwa hivyo tunaweza kuishi katika uhusiano naye. Kwa hiyo tunaweza kuwa Watu wake. Sasa na hata milele.”

Kuna mengi zaidi kwenye Hadithi hii Kuu. Katika wiki zijazo tutafurahia ufunuo wa Hadithi hii ya ajabu. Lakini kwa sasa, angalia saa yako.

Angalia ikiwa nilifanya nilivyoahidi ndani ya dakika 5. ☺

Ubarikiwe sana katika jina la Yesu.

Ni wako

Douglas

Douglas Van Davender.

Huduma za 'Jesus Ministries International' na 'Transforming Prayer'.